Neno “kuguguna” linapatikana mara moja tu katika kitabu cha *Ayubu 30:3* na maana yake ni *“kutafuna”*

> *Ayubu 30: 2 “Naam, uwezo wa mikono yao utanifaa nini? Watu ambao nguvu zao zimekoma.*
>
> *3 Wamekonda kwa uhitaji na njaa; HUGUGUNA NCHI KAVU, penye giza la ukiwa na uharibifu”*

Hapa maandiko yanalizungumzia kundi la watu ambao ni maskini, wasio na nguvu, huguguna (hutafuna) riziki zao mahali pakame, penye giza na uharibifu.

Ufunuo kamili kwa mtu yule anayemtegemea mwanadamu.. Maandiko yanasema atakaa mahali pakame, katika nchi ya chumvi..

> *Yeremia 17:5 “ Bwana asema hivi, AMELAANIWA MTU YULE AMTEGEMEAYE MWANADAMU, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana.*

> *6 Maana atakuwa kama FUKARA NYIKANI, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani PALIPO UKAME, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu."*

Bwana atusaidie tumtegemee yeye siku zote, na kumfanya yeye kuwa kinga yetu.

Maran atha.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Hazama ni nini katika biblia?(Ezekieli 16:12, Kutoka 24:47)

RACA

Kuguguna maana yake nini? (Ayubu 30:3 )

HAMA KUTOKA GIZANI

Bwana alimaanisha nini kusema “kila mtu atatiwa chumvi kwa moto”

Mapooza ni nini? Na je! Twawezaje kuepukana nayo?

Rudi nyumbani

Share on:
WhatsApp